# LONDA

## NAMIBIA HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE





# RIPOTI YA 2020

PARADIGM INITIATIVE

www.paradigmhq.org

@ParadigmHQ

# LONDA

## NAMIBIA HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI 2020 RIPOTI

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE

**Imechapishwa na Paradigm Initiative**
374 Borno Way, Yaba, Lagos, Nigeria
Email: media@paradigmhq.org
www.paradigmhq.org

Iliyochapishwa mnamo Aprili 2021

Ripoti iliyotolewa na Nashilongo Gervasius
Timu ya Uhariri: 'Gbenga Sesan, Kathleen Ndongmo, Koliwe Majama, Margaret Nyambura Ndung'u, Mawaki Chango, Nnenna Paul-Ugochukwu and Thobekile Matimbe.
Ubunifu na Luce Concepts

This publication may be reproduced for non-commercial use in any form provided due credit is given to the publishers, and the work is presented without any distortion.

Copyright © 2021 Paradigm Initiative

Creative Commons Attribution 4.0 International (CC BY 4.0)



# LONDA

**NAMIBIA HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI 2020 RIPOTI**

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE

Asasi za kiraia zinaendelea kufanya kazi ili kuendeleza haki za dijitali na ujumuishi barani Afrika, kuhakikisha njia bora zinapitishwa katika sera na sheria. Ripoti hii inachambua hali ya haki za dijitali na ujumuishi nchini Namibia, ikichunguza ukiukaji na mapungufu, ikiangazia utumiaji na utekelezwaji wa sera na sheria, ikiangazia hatua muhimu na kutoa mapendekezo kwa mandhari ya dijitali nchini Namibia. Pamoja na ripoti kutoka nchi 20, toleo hili linaangazia kati ya maswala mengine, pengo la kidijitali lililozidishwa na janga la COVID-19 na kufichua ukiukaji kwenye nyanja tofauti kama vile faragha, ufikiaji wa habari, na uhuru wa kujieleza na msingi wa sheria na sera ulioelezewa vizuri .

PARADIGM INITIATIVE

@ParadigmHQ

## YALIYOMO

UTANGULIZI 1

KUFURAHIA UHURU WA KUJIELEZA MTANDAONI 2

ATHARI YA COVID-19 KWA HAKI ZA KIDIJITALI NA UJUMUISHI 2

UFIKIAJI MTANDAO 3

FARAGHA, UTAMBULISHO WA KIDIJITALI NA UFUATILIAJI 3

MATAMSHI YA CHUKI, TAARIFA POTOFU NA SHERIA ZA MAKOSA YA JINAI 5

KIWANGO CHA KUTENGWA KIDIJITALI NA ATHARI ZAKE KWA HAKI ZA BINADAMU 5

MIUNDOMBINU YA KIDIJITALI 6

JINSIA NA TEHAMA 6

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 7



Namibia ni nchi iliyoko Kusini mwa Afrika yenye idadi ya watu milioni 2.5. Baada ya kupata uhuru wake mwaka 1990, demokrasia kwa ujumla inaonekana kustawi na sheria kuzingatiwa. Ingawa ni nchi ya uchumi wa kati, Namibia ina mojawapo viwango vya juu zaidi vya ukosefu wa usawa wa mapato ulimwenguni.[1]

UTANGULIZI

# HAKI ZA DIJITALI NA UJUMUISHAI YA NCHI YA NAMIBIA

Kipengele cha 21 cha Katiba ya Jamhuri ya Namibia kinahakikishia "uhuru wa kusema na kujieleza, ambao utajumuisha uhuru wa vyombo vya habari na vyombo vingine vya habari," ikitoa vizuizi halali chini ya 21 (2) ikiwa ni pamoja na sababu za "usalama wa kitaifa, utulivu wa umma, adabu au maadili, kudharau mahakama, kukashifu au kuchochea."[2] Kwa miaka Namibia imefurahia kiwango cha juu zaidi barani Afrika kwenye faharasa ya uhuru wa vyombo vya habari ulimwenguni, na kuboreshwa kwa kiwango kutoka 26 katika 2018 hadi 23 katika 2019 na 2020 kati ya nchi 180 zilizofanyiwa utafiti.[3]




Takwimu za Muungano wa Kimataifa wa Technolojia ya Mawasiliano (ITU) zinaonesha kuwa, mnamo 2014, 35.5 kwa kila wakazi 100 walikuwa na usajili wa mtandao wa rununu[4] na kufikia 2018 idadi hiyo ilikuwa imeongezeka hadi 59.3 katika kila 100[5] Ripoti ya ya Jumuiya ya Habari ya 2018 iliita Namibia "mmoja wa watangulizi barani Afrika juu ya maendeleo ya TEHAMA".[6] Pamoja na kukua kiwango cha kidijitali, ni muhimu zaidi kwa uhuru wa kimsingi kulindwa mtandaoni na nje ya mtandao.

1. 'Namibia Overview', https://www.worldbank.org/en/country/namibia/overview
2. Constitution of the Republic of Namibia, https://www.constituteproject.org/constitution/Namibia_2010.pdf
3. RSF, https://rsf.org/en/namibia
4. Measuring the Information Society Report 2015, https://www.itu.int/en/ITUD/Statistics/Documents/publications/misr2015/MISR2015-w5.pdf
5. Measuring the Information Society Report 2018, https://www.itu.int/en/ITU-D/Statistics/Documents/publications/misr2018/MISR-2018-Vol-2-E.pdf
6. Measuring the Information Society Report 2018, p.126, https://www.itu.int/en/ITU-D/Statistics/Documents/publications/misr2018/MISR-2018-Vol-2-E.pdf

## KUFURAHIA UHURU WA KUJIELEZA MTANDAONI

Haki za binadamu mtandaoni, haswa haki ya faragha, uhuru wa kujieleza, uhuru wa maoni na haki ya kupata habari, ni baadhi ya maswala muhimu kwenye haki za kidijitali na ujumuishaji katika muktadha wa Namibia.


Mitandao ya kijamii inazidi kutumiwa kuelezea maoni mbadala, na katika kulenga kulidhibiti hili, wanasiasa wamekuwa wakitoa wito wa kuidhibiti mitandao ya kijamii kama njia mojawapo ya kupambana na habari potofu na uhalifu wa mtandaoni.[7] Kwa miaka michache iliyopita, wanasiasa na maafisa wa serikali wametoa onyo kali na vitisho wakitaja "matumizi yasiyofaa"[8] ya mitandao ya kijamii, huku wakidai kuwa inahatarisha maisha.[9]

Pendekezo la kudhibiti mitandao ya kijamii linasemekana kuzua mgawanyiko miongoni mwa wabunge 2019.[10] Hata hivyo, mnamo Februari 2020, Wizara ya TEHAMA ilithibitisha mipango ya kuidhibiti[11] Ingawa serikali inadai kwamba kanuni hizo zinapania tu kuzuia uchombezaji wa wasichana wa shule, hatua kama hizi zinaweza kuonekana kusababisha kizuizi kisichohitajika kwa uhuru wa kujieleza mtandaoni.

## ATHARI YA COVID -19 KWA HAKI ZA KIDIJITALI NA UJUMUISHI

Mnamo Aprili 2020, kama sehemu ya kanuni za kuzuia kuenea kwa COVID-19, Namibia ilipiga marufuku uchapishaji wa taarifa za uwongo au za kupotosha zinazohusiana na virusi, ikiwemo kwenye mitandao ya kijamii.[12] Kufuatia hili mwanamume mmoja alikamatwa chini ya kanuni hii mnamo Juni.[13]

Mnamo Aprili 2020, serikali ya Namibia ilizindua elimu kwa njia ya mtandao nchini kote kama hatua ya kudhibiti janga hilo.[14] Uamuzi huu umekosolewa kwani nchi ina mpango duni wa teknolojia chini, na ni 30% tu ya shule ambazo zina mtandao.[15]




7. 'Vice president wants to censor social media', https://www.namibiansun.com/news/vice-presidentwants-to-censor-social-media
8. 'Government warns against irresponsible use of social media', https://neweralive.na/posts/govt-warns-against-irresponsible-use-of-social-media
9. 'Social media endangers lives', https://www.namibiansun.com/news/social-media-endangerslives/
10. 'MPs divided on social media gagging', , https://www.namibian.com.na/190767/archive-read/MPs-divided-on-social-media-gagging,
11. 'Govt mulls social media protection', https://www.namibian.com.na/197767/archive-read/Govt-mulls-social-media-protection
12. 'Covid-19 'fake news' now a crime, https://www.namibian.com.na/200224/archive-read/Covid19-fake-news-now-a-crime
13. 'Man arrested for spreading fake Covid-19 news', https://www.namibian.com.na/91561/read/Man-arrested-for-spreading-fake-Covid-19-news
14. 'Govt ponders e-learning for schools', https://www.namibian.com.na/199902/archive-read/Govt-ponders-e-learning-for-schools
15. '70% of Govt schools without internet', https://allafrica.com/stories/201910080121.html

Jarida la Julai 2020 na Muungano wa Mawasiliano Endelevu – Association for Progressive Communication(APC) umeonyesha kuwa hatua hiyo ilileta "vipengele vikubwa vya kibaguzi kwa wale ambao hawajaunganishwa na hawawezi kumudu mtandao, na iliingilia haki ya maendeleo na ufikiaji wa elimu, kanuni iliyopo kwenye Azimio la Afrika kuhusu Haki na Uhuru wa Mtandaoni."[16]

Kulikuwa na hitilafu kubwa katika ulindaji data wakati wa COVID-19, na matukio yaliyoripotiwa ya wanawake walioripoti kupokea mawasiliano kutoka kwa wanaume wasiowajua ambao walidai kuwa walipata nambari zao za simu kutoka kwa vituo vya usajili vilivyoanzishwa kama hatua za kufuatilia mawasiliano. Vyombo vya habari vikiripoti kisa cha wizi wa daftari la usajili,[17] na pia kuashiria kwamba watu wengi walikuwa wakitumia majina yasiyo ya kweli katika rejista hizi, labda kutokana na wasiwasi wa usalama.[18] Miezi tisa baada ya uzinduzi wazo, serikali imefutilia mbali hitaji la usajili wa wateja katika maeneo ya umma ikitaja ukosefu wa ukweli wa taarifa zinazotolewa.[19]

## UFIKIAJI MTANDAO

Sekta ya teknolojia ya Namibia inazuiliwa na ukosefu wa upatikanaji wa bei nafuu, na huduma duni.[20]Kielelezo cha Mtandao Jumuishi cha 2020, ambacho kinachunguza upatikanaji wa mtandao, upatikanaji wa bei, umuhimu wa yaliyomo na utayari, imeweka Namibia nafasi ya 84 kati ya nchi 100, na alama ya 41.2% ya upatikanaji na 54.8% kwa viashiria vya ununuzi mtawaliwa. Takwimu za ITU zinaonyesha kuwa, kufikia Juni 2018, asilimia ya watu wanaotumia mtandao nchini Namibia ni 36.8%[21] ikilinganishwa na 14.8% mnamo 2014.[22]

Sera ya Kitaifa ya vifurushi (Broadband) ilizinduliwa mwanzoni mwa 2020 kwa lengo la kuafikia huduma za kutegemewa na zenye bei nafuu za ufikiaji wa broadband kwa wote.[23] Mpango wa utekelezaji wa sera ya miaka mitano inaazimia kuhakikisha ufikiaji wa 95% ya broadband ifikapo mwaka 2024, na pia kutekeleza Mfuko wa Ufikiaji Huduma kwa wote (Universal Access Fund).[24]

## FARAGHA, UTAMBULISHO WA KIDIJITALI NA UFUATILIAJI

Wakati haki ya faragha imetolewa chini ya Kifungu cha 13 cha Katiba ya Namibia,[25] nchi hiyo bado haina sheria ya ulindaji data na faragha. Hata hivyo, kuna dalili za maendeleo katika swala hili, kwani serikali kwa sasa inaandaa sera ya kulinda data.[26] Mnamo Februari 2020, mashauriano ya wadau mbalimbali yalifanyika[27]na mashauriano zaidi ya wadau kuhusu Muswada uliopendekezwa yalifanywa kati ya Septemba na Oktoba.[28] Na ukosefu wa sheria ya ulindaji data, ukiukaji wa data umeripotiwa hata kutoka hifadhi data za serikali.[29] Nchi hiyo imeitwa "mahali salama kwa uhalifu wa mtandaoni",[30] na bila

16. Compulsory e-learning in Namibia's public schools, https://africaninternetrights.org/sites/default/files/Nashilongo_Gervasius.pdf
17. 'Covid-19 customer register stolen', https://www.namibian.com.na/206001/archive-read/Covid-19-customer-register-stolen
18. First name 'Apple', last name 'Tomato', https://www.namibian.com.na/96668/read/First-name-Apple-last-name-Tomato
19. Govt to tighten COVID -19 rules https://www.namibian.com.na/97414/read/Govt-to-tighten-Covid-19-rules
20. 'Namibia's internet costs are too high', https://www.namibiansun.com/news/namibias-internetcosts-are-too-high2019-03-05,
21. Measuring the Information Society Report 2018, https://www.itu.int/en/ITUD/Statistics/Documents/publications/misr2018/MISR-2018-Vol-2-E.pdf
22. Measuring the Information Society Report 2015, https://www.itu.int/en/ITUD/Statistics/Documents/publications/misr2015/MISR2015-w5.pdf
23. 'Namibia launches national broadband policy, https://southerntimesafrica.com/site/news/mict-namibia-launches-national-broadband-policy
24. 'Govt targets 95% broadband coverage by 2024', https://neweralive.na/posts/govt-targets-95-broadband-coverage-by-2024
25. Namibian Constitution, https://www.lac.org.na/laws/annoSTAT/Namibian%20Constitution.pdf
26. 'Data Protection Laws of the World', https://www.dlapiperdataprotection.com/index.html?t=law&c=NA#:~:text=The%20Namibian%20Government%20is%20currently,of%20their%20personal%20data%2C%20and
27. 'GLACY+: Stakeholders' Consultation Workshop on the Data Protection Bill in Namibia', https://www.coe.int/en/web/cybercrime/-/glacy-stakeholders-consultation-workshop-on-the-data-protection-bill-in-namibia
28. Highlights for September pg14x- Council of Europe https://rm.coe.int/cybercrime-coe-update-2020-q3/16809fd8fa
29. 'SSC leak exposes personal info online', https://www.namibian.com.na/178310/archive-read/SSC-leak-exposes-personal-info-online
30. 'Namibia a safe haven for cybercriminals', https://neweralive.na/posts/namibia-a-safe-haven-for-cybercriminals



> ***Sera ya Kitaifa ya vifurushi (Broadband) ilizinduliwa mwanzoni mwa 2020 kwa lengo la kuafikia huduma za kutegemewa na zenye bei nafuu za ufikiaji wa broadband kwa wote.***

sheria ya uhalifu wa mtandaoni,[31] raia wengi wamejikuta wahanga wa kuandaliwa kingono, visasi vya ngo na utapeli wa mtandaoni.[32]

Mnamo mwaka wa 2017, Mamlaka ya Mawasiliano ya Namibia (CRAN) ilitekeleza kifungu ndani ya Sheria ya Mawasiliano ya 2009 inayohitaji usajili wa lazima wa kadi za simu kupitia waendeshaji wa mawasiliano.[33] Zoezi la usajili baadaye lilitelekezwa wakati asasi za kiraia na vyombo vya habari viliibua wasiwasi.[34] Hata hivyo, kanuni za kadi za simu zinaweza kuangaliwa upya kama sehemu ya uhakiki unaoendelea wa Sheria ya Mawasiliano.[35]

Sehemu ya 6 ya Sheria ya Mawasiliano inatoa nguvu mbali mbali za kuteka mawasiliano, na kifungu cha 70 (1) kinatoa mwongozo wa sheria ya kuanzisha kituo cha kuteka mawasiliano kwa madhumuni ya usalama wa kitaifa na kupambana na uhalifu.[36]

Kwa jumla, kuna dhana kwamba ufuatiliaji unaofadhiliwa na vyombo vya dola miongoni mwa asasi za kiraia na vyombo vya habari, haswa na Kitengo cha Ujasusi, kama ilivyoripotiwa na gazeti la Namibia katika makala ya kina ya sehemu tatu.[37]

31. 'Cybercrime in Namibia', https://www.namibian.com.na/165301/archive-read/Cybercrime-in-Namibia
32. 'Many Namibians fall victim to online fraud', https://www.nbc.na/news/many-namibians-fall-victim-online-fraud.20124
33. 'Spy agency wants SIM cards registered', https://www.namibian.com.na/163120/archive-read/Spy-agency-wants-SIM-cards-registered
34. 'Ripe for surveillance abuse – Unpacking Namibia's SIM card registration limbo', https://action-namibia.org/ripe-for-surveillance-abuse-unpacking-namibias-sim-card-registration-limbo/
35. 'Namibia undertakes review of communications law', https://www.commsupdate.com/articles/2019/10/11/namibia-undertakes-review-of-communications-law/
36. Communications Act, 2009, https://www.nbc.na/sites/default/files/pdf/Namibia%20Communications%20Act%208%20of%202009_0.pdf
37. Action Access to Internet, 'The rise of the Namibian surveillance state (Part I)', https://action-namibia.org/rise-namibian-surveillance-state/; 'The Rise of the Namibian Surveillance State: Part 2', https://www.namibian.com.na/174788/archive-read/The-Rise-of-the-Namibian-Surveillance-State-Part-2; ; 'The rise of the Namibian surveillance state: Part 3', https://www.namibian.com.na/175475/archive-read/The-rise-of-the-Namibian-surveillance-state

## MATAMSHI YA CHUKI, TAARIFA POTOFU NA SHERIA ZA MAKOSA YA JINAI

Wakati uhuru wa kusema umehakikishiwa kikatiba, ulinzi wa kikatiba kwa usalama wa taifa, utulivu wa umma, na maadili ya umma hutoa sababu za kisheria za kuzuia uhuru wa vyombo vya habari.[38] Kukashifu ni kosa la jinai chini ya sheria ya kawaida, na kumekuwa na kesi kadha za ukashifu mahakamani zilizofanikiwa.[39]

Ubaguzi wa rangi kwa sasa unadhibitiwa chini ya Sheria ya Kupinga Ubaguzi wa Rangi ya 1991.[40] Hata hivyo, matamshi ya chuki nchini Namibia hayajapigwa marufuku, na mnamo 2008 shirika la Umoja wa Mataifa (UN) lilikosoa nchi hiyo kwa kutopiga marufuku matamshi ya chuki, haswa kwa vikundi vya watu wachache.[41]

Taarifa potofu zinazohusiana na COVID-19 zimepigwa marufuku hivi karibuni na adhabu yake ni faini ya hadi Dola za Namibia 2,000 (USD 134) au kifungo cha hadi miezi sita gerezani.[42]

## KIWANGO CHA KUTENGWA KIDIJITALI NA ATHARI ZAKE KWA HAKI ZA BINADAMU

Mtandao ni ghali sana na ukosefu wa ufikiaji wake nchini Namibia unawaacha wengi wametengwa kidijitali.[43] Utafiti uliofanywa na Alliance for Affordable Internet (A4AI) mnamo 2019 umebaini kuwa GB1 ya data nchini Namibia iligharimu Dola 8.57 za Marekani (USD).[44] Telecom Namibia inatoza Dola 139.00 za Namibia (N$)kwa GB1 ya inayolipwa kabla (prepaid), sawa na Dola 9.32 za Marekani (USD)[45] Kumekuwepo na mafanikio kuelekea ujumuishaji kidijitali. Katika mpango mkakati wake wa 2017/22, Wizara ya TEHAMA (MICT) ililenga kuhakikisha mtandao wa simu za rununu na mtandao "hadi pembe zote za nchi" (uk. 23).[46] MICT pia ilianzisha vituo 25 vya jamii vyenye malengo anuwai katika maeneo ya vijijini nchini Namibia, vyenye miundombinu tosha ya mtandao (uk. 2).[47]

Mnamo mwaka wa 2016, MICT ilijitolea kulipatia taifa lote mtandao wa simu ya rununu kufikia katikati ya mwaka wa 2020, ili kufanya taarifa zipatikane zaidi, zenye bei nafuu na zinazofaa, kupitia mpango uliotekelezwa na shirika la simu la Telecommunications Limited (MTC).[48] Kama sehemu ya mpango huu, MTC inakusudia kujenga minara mipya 500 nchini kote.[49]

Kutengwa kidijitali kunaiathiri sana sekta ya elimu, ambapo 70% ya shule za serikali hazijaunganishwa kwenye mtandao.[50] Naibu Waziri wa Elimu, Sanaa na Utamaduni alithibitisha kuwa, kati ya shule 1,897 za serikali kote nchini, ni shule 590 tu zimeunganishwa kwenye mtandao.[51]

> *"Kukashifu ni kosa la jinai chini ya sheria ya kawaida"*

38. Constitution of the Republic of Namibia, https://www.constituteproject.org/constitution/Namibia_2010.pdf
39. For example, 'Hamata to pay for defamation', https://www.namibian.com.na/119662/archive-read/Hamata-to-pay-for-defamation; https://namiblii.org/na/judgment/high-court-main-division/2017/103
40. https://laws.parliament.na/annotated-laws-regulations/law-regulation.php?id=375
41. 'UN report lambasts Nam for hate speech', https://www.namibian.com.na/41758/archive-read/UN-report-lambastes-Nam-for-hate-speech
42. Covid-19 fake news now a crime', https://www.namibian.com.na/200224/archive-read/Covid19-fake-news-now-a-crime
43. 'Namibia's Internet Costs are too High', https://www.namibiansun.com/news/namibias-internet-costs-are-too-high2019-03-05
44. The Alliance for Affordable Internet, https://a4ai.org/extra/mobile_broadband_pricing_usd-2019Q2
45. https://internetpkg.com/namibia-internet-packages/
46. Ministry of Information and Communication Technology (MICT) 2017/22 Strategic Plan, p.23, http://www.mict.gov.na/documents/32978/266786/MICT+STRATEGIC+PLAN+2017-2022/3596bd32-0aa5-498a-b4c9-b396af9e8c1a
47. Ministry of Information and Communication Technology (MICT) 2017/22 Strategic Plan, p.2, http://www.mict.gov.na/documents/32978/266786/MICT+STRATEGIC+PLAN+2017-2022/3596bd32-0aa5-498a-b4c9-b396af9e8c1a
48. 'MTC aims to connect 20 000 in rural areas', https://neweralive.na/posts/mtc-aims-connect-20-000-rural-areas
49. 'MTC to erect 500 new towers', https://www.namibian.com.na/174168/archive-read/MTC-to-erect-500-new-towers
50. 'Namibia: 70 Percent of Govt Schools Without Internet', https://allafrica.com/stories/201910080121.html
51. '32% of public schools not equipped for online learning', https://www.telecom.na/media-centre/212-internet-exchange-point-launched-in-windhoek



## MIUNDOMBINU YA KIDIJITALI

Kwa msaada wa Jumuiya ya Afrika na Ofisi ya Afrika ya Shirika la Mtandao (Internet Society), Namibia ilizindua Kituo cha Kubadilishana Intaneti (IXP) mnamo 2014.[52] Utendaji wa kituo hiki haujaamuliwa kwani hakuna mengi yaliyoandikwa kukihusu. Walakini, kulingana na Paulina Magongo, mjumbe wa kamati inayosimamia IXP, IXP ya eneo hili imekuwa ikikabiliwa na changamoto kutoka 2017 na kwa muda sasa, vifaa vyake vimekaribia kupitwa na wakati.[53]

Miundombinu mingine ya TEHAMA nchini Namibia pia ni pamoja na Mfumo wa Mkonga wa Magharibi mwa Afrika (WACS) uliowasili nchini mwanzoni mwa 2011.[54] Uwepo wa mkonga huu wa mawasiliano nchini ulipaswa kuleta mtandao wa bei nafuu na kuleta manufaa mengi katika sekta ya TEHAMA ya uchumi wa Namibia, lakini nyaya hizo zimeripotiwa kuharibiwa mara kadha tangu kusimikwa kwake.[55]

Kielelezo cha Mtandao Jumuishi cha 2020 kimeorodhesha Namibia kwa jumla katika nchi 84 kati ya 100 zilizotafitiwa na kuiweka nchi hiyo kwa 21.2% kwenye kitengo cha miundombinu, ikionyesha kwamba wakati nchi hiyo imefunikwa kwa 100% na mtandao wa 2G, mtandao wa 3G unashughulikia 53% tu ya nchi hiyo wakati chanjo ya mtandao wa 4G iko chini zaidi kwa 39% bila upelekaji wa 5G ulioripotiwa. Ripoti hiyo imekadiria Namibia 0 (sifuri) juu ya viashiria kuhusu mipango ya serikali na sekta binafsi ili kufanya Wi-Fi ipatikane.[56]

Kifungu cha 57 cha Sheria ya Mawasiliano ya 2009 (Sheria Na. 8 ya 2009) kinataja kuanzishwa kwa Mfuko wa Huduma kwa Wote, unaotekelezwa chini ya CRAN na kufadhiliwa na ushuru wa mauzo ya waendeshaji wenye leseni.[57] Walakini, mfuko huo haujawahi kufanya kazi kwani Mahakama Kuu iliamua mnamo 2018 kuwa ukusanyaji wa ushuru huo ulikuwa kinyume cha katiba.[58]

## JINSIA NA TEHAMA

Kielelezo cha Mtandao Jumuishi cha 2020 kiliripoti kuwa pengo la jinsia la Namibia katika ufikiaji mtandao limefikia 14.1%, na 64% ya wanaume na 55% ya wanawake wakiwa watumiaji wa mtandao.[59] Mnamo mwaka wa 2012, ni 25.8% tu ya wanawake walikuwa na simu ya rununu inayowezeshwa na mtandao ikilinganishwa na 36.9% ya wanaume.[60]

Jamii ya wanawake katika teknolojia ipo nchini Namibia, ingawa nyanja hiyo inaendelea kutawaliwa na wanaume. Walakini, watengenezaji

52. 'Internet Exchange Point Launched in Windhoek', https://www.telecom.na/media-centre/212-internet-exchange-point-launched-in-windhoek
53. Telephonic Interview, November 18, 2020, Paulina Magongo
54. 'WACS Submarine Cable Lands in Swakopmund Today', https://www.telecom.na/media-centre/260-wacs-submarine-cable-lands-in-swakopmund-today
55. 'WACS undersea cable damaged again', https://www.we.com.na/news/wacs-undersea-cable-damaged-again2020-03-30
56. The Inclusive Internet Index 2020, https://theinclusiveinternet.eiu.com/explore/countries/NA/
57. Government Gazette 8 June 2015, https://www.lac.org.na/laws/2019/6886.pdf
58. 'Supreme Court rules against Cran levy', https://www.namibian.com.na/68353/read/Supreme-Court-rules-against-Cran-levy
59. The Inclusive Internet Index 2020, https://theinclusiveinternet.eiu.com/explore/countries/NA/performance/indicators/
60. 'Lifting the Veil on Gender ICT Indicators in Africa', p.29, https://www.researchictafrica.net/publications/Evidence_for_ICT_Policy_Action/Policy_Paper_13_-_Lifting_the_veil_on_gender_ICT_indicators_in_Africa.pdf

wa kike wanaripotiwa kuwa sehemu ya mduara wa watengenezaji programu wa Google na Facebook.[61] Hivi karibuni kikundi cha wanawake wadukuzi kilishinda tuzo la ubunifu lililoandaliwa na UNDP.[62]

Ripoti ya Haki za Wanawake mtandaoni ya 2020 kuhusu Namibia[63] iliipa nchi alama ya 29% kulingana na tathmini yake katika kategoria za ufikiaji mtandao na uwezeshaji wa wanawake; umuhimu wa maudhui na huduma; usalama mtandaoni; kumudu; na ujuzi na elimu ya kidijitali. Ripoti hiyo inaonyesha kuwa ni 47% tu ya wanawake wa Namibia wanaofikia mtandao na kwamba hakuna sera ya kitaifa inayotambua teknolojia kama nyenzo ya kupambana na pengo la usawa wa kijinsia. Ukatili wa mtandaoni dhidi ya wanawake pia unasalia kuwa changamoto.[65] Ripoti Wanawake mtandaoni ya 2020 pia inaonyesha kwamba ukosefu wa sheria ya uhalifu wa mtandaoni na ulindaji data nchini Namibia unawaweka wanawake katika hatari ya unyanyasaji na katika mazingira magumu, katika visa vya kushiriki picha bila kibali (pia inayojulikana kama ngono au ponografia ya kulipiza kisasi), na vile vile usaliti mtandaoni na matamshi ya chuki ya kijinsia.[65]

Wanawake kwenye nyadhifa kuu na maarufu huwa wanalengwa wa unyanyasaji na uonevu mtandaoni. Jamii ya Mtandao Namibia (Internet Society Namibia Chapter) mnamo 2019 iliandaa Jukwaa la Kidijitali kwa Wanawake katika nafasi za Kisiasa na Maarufu iliyolenga kuwashirikisha na kuwawezesha wanawake na ujuzi wa kupunguza unyanyasaji mtandaoni.[66]

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Namibia inajizatiti kwenye ujumuishaji mkubwa zaidi wa kidijitali, na pia inajitahidi kuelekea kwenye ulindaji data na uhalifu wa mtandaoni. Licha ya hili, hadi wa leo mizani imepinda sana na kuegemea udhibiti na uingiliaji wa serikali, huku hatua chache sana zikichukuliwa kuhakikisha usalama wa kweli wa raia wake na uunganishwaji kwenye mtandao. Maswala yanayohusiana na jinsia na teknolojia yanahitaji ushughulikiwaji wa upesi, kwani wanawake wanakabiliwa na athari za mtandaoni na wakati huo huo wana kuna uwezekano mkubwa wa wao kutengwa kidijitali.

Kwa kutamatisha, mapendekezo yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa;

**Miundombinu:** Jitihada kubwa zinahitaji kutekelezwa katika kufanya uhamasisho wa faida na matumizi ya IXP ndani ya nchi na jinsi inavyotafsiri kuwa maswala ya kiuchumi na usalama wa mtandao. Kuna haja ya kutafsiri faida ya WACS kwa nchi na jinsi hili linavyotafsiri katika uunganishwaji mkubwa wa nchi.

61. Namibia Women inTech; https://namtechwomen.com/about-us
62. 'Female 'hackers' take the lead', https://www.we.com.na/news/female-hackers-take-the-lead2020-08-18/
63. 'Women's rights online report', http://webfoundation.org/docs/2020/08/GenderReport-Namibia.pdf
64. 'Addressing 'Revenge Porn' in Namibia', https://ohrh.law.ox.ac.uk/addressing-revenge-porn-in-namibia/
65. Women's rights online report' http://internetsociety.na/wpcontent/uploads/2020/07/GenderReport-Namibia-FINAL-ONLINE-VERSION.pdf
66. 'Call for anti-online bullying law', https://www.namibian.com.na/84148/read/Call-for-anti-online-bullying-law

Namibia lazima ifanye kazi ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (Universal Service Access Fund) kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mawasiliano ili kufanikisha upatikanaji sawa wa mtandao.

**Ushirikishwaji kidijitali:** Namibia inapaswa kupitisha bei ya Tume ya Broadband ya Shirika la Umoja wa Mataifa (UN) ya GB1 ya data ya rununu iliyowekwa isiyozidi bei ya 2% ya kipato cha kila mwezi cha GNI kwa kila mtu. Sekta zote za serikali na za kibinafsi zinapaswa kufanya Wi-Fi kupatikana katika maeneo ya umma na kwa kuongeza Serikali inapaswa kuhakikisha unganishwaji wa shule zote kwenye Mtandao. Mpango wa utekelezaji wa Tume ya Broadband unahitaji kutathminiwa kwa karibu ili kuhakikisha mafanikio ya ufikiaji wa broadband kote nchini.

**Faragha na Ulindaji Mtandaoni:** Na Muswada wa Ulindaji wa Data za umma unaosemekana kutayarishwa na Muswada wa Uhalifu wa Mtandaoni unaelekea kukamilika, nchi inapaswa kuhakikisha ulindaji na faragha ambayo inalinda raia haswa wanawake na jamii zingine zilizo hatarini.

**Mitandao ya Kijamii:** Kuna ushahidi kwamba mitandao ya kijamii imewezesha uhusikaji zaidi katika mijadala ya umma na pia kuruhusu kuongezeka kwa ufikiaji na kushiriki habari. Kwa ujumla mitandao ya kijamii pia imeongeza matumizi ya mtandao nchini. Kwa kuzingatia maendeleo haya na mengineyo, mazungumzo ya kudhibiti mitandao ya kijamii yanapaswa kusitishwa.

# LONDA

## NAMIBIA HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI 2020 RIPOTI

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE

PARADIGM INITIATIVE

**Paradigm Initiative**

374 Borno Way, Yaba, Lagos, Nigeria

Email: media@paradigmhq.org

www.paradigmhq.org

@ParadigmHQ